# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL5

# KISWAHILI PAPER 2 QUESTIONS

## 1. UFAHAMU (Alama 15 )

### Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

1. Wazazi wetu wapenzi, waalimu, wanafunzi wenzangu mabibi na mabwana. (Anawainamia). Niko mbele yenu kuwatolea wasilisho juu ya umuhimu wa kupanga uzazi. Ni lazima niwahakikishie kwamba sikuchukuliwa vivi hivi katika safari hii. Ni safari niliyopatiwa wasaa wa kujitayarisha na sasa naamini kuwa njia yake naielewa.

Suala la upangaji wa uzazi limezusha kutoelewana kwa kiasi Fulani, wananchi wengi wakifikiria kuwa kupanga uzazi ni kuacha kuzaa. Hata kidogo jamani tuache kuzaa kisha tuiachie nani dunia tuliyoirithishwa na Muumba wetu? Mpango wa uzazi unamaanisha kuwa watu wazae watoto wanaoweza kuwalea. Hivi ni kusema kwamba, ikiwa uwezo wa jamii Fulani ni kulea mtoto mmoja, jamii hiyo izae mtoto mmoja. Ikiweza kutunza watoto wawili, watatu, hakuna ubaya kuwazaa.

Fauka ya hayo, nchi ambayo haizingatii mpango wa uzazi, kila familia ikijipatia takribani timu ya kandanda, hukumbwa na matatizo chungu mbovu. Baadhi ya matatizo hayo ni kama vile mipango ya maendeleo (kupitia huduma mbalimbali) kutoweza kuoana na hali halisi ya nchi. Mathalan, nafasi za kazi huadimika, chakula huwa hakitoshi, milolongo ya wagonjwa hospitalini huendelea kuzidi urefu huku madaktari wakilazimika kupurukusha kazi. Katika hali ambapo watu wanazaa kwa wingi, wazururaji nao huleta magonjwa ya zinaa. Lazima tujihadhari. Kuna ukimwi ambao ni nduli. Mbali na haya, uzazi bila mpango pia huongeza ukora na uhuni wa wizi, ujambazi, ulanguzi, ukampunisinzia, uombaji wa bandia, na kadhalika.

Aidha mpango wa uzazi unamaanisha watoto kuzaliwa kwa majira. Uzazi wa majira ni muhimu katika kutunza afya ya mama, la sivyo itadhoofika haraka mno. Muda wa kupumua kwake humwezesha kurudisha nguvu mwilini. Jambo hili haliwezekani wakati mama anapata mtoto kila baada ya miezi sita (kicheko). Kwanza watoto wenyewe hawawezi kukua kwa afya. Vitoto vinavyozaliwa unyounyo kama kwamba kuna mashindano huwa vidhoofu, vikishuhudiisha ukosandisha, nguo zao zikiwa mararu tu. Hii ni aibu siyo tu kwa wazazi bali pia kwa nchi nzima kwa jumla. Kama kuzaa kungekuwa kwa zamu, yaani mke akizaa mwaka huu, mume azae mwaka mwingine (kicheko na makofi), kama mambo yangekuwa hivi, nina hakika kwamba yangeeleweka vizuri sana na kwa urahisi, haya ninayojaribu kuyasisitiza.

Wazazi wapenzi, waalimu, wanafunzi wenzangu, mabibi na mabwana. Shoka liso mpini haliwezi kuchanja kuni. Ni lazimai niwashukuru sana waalimu wangu walionitayarisha na kunijasirisha kiasi cha kuweza kusimama mbele yenu. Natoa shukrani za dhati kwenu nyote kwa heshima mliyonitunukia hata ijapokuwa mnashuhudia kwamba nywele zangu bado ni nyeusi tititi. Ahsanteni sana. (Makofi).

Maswali

.a) Kulingana na taarifa hii kupanga uzazi kunamaanisha mambo matatu. Yataje

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

b) Katika methali ya shoka liso mpini halichanji kuni, kama ilivyotumiwa na mwandishi, ni nani ‘shoka’ na ni nani “mpini”?

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

c) Mwandishi anamaliza hotuba yake kwa kuishukuru hadhira kwa kumtunukia heshima, hata ijapokuwa nywele zake ni nyeusi tititi i) Ametunukiwa heshima gani?

…………………………………………………………………………………………………

ii) Ni ujumbe gani hasa anaonuia kutoa katika kusema kuwa nywele zake ni nyeusi tititi?

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

d) Katika habari hii, mwandishi anajitokeza kama msemaji wa mizaha ya mara kwa mara kupitia matumizi yake ya lugha. Taja mifano mitatu ya mizaha hiyo

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

e) Eleza matumizi ya lugha yafuatayo kama yanavyodhihirika katika taarifa hii

i) Mathalan

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

ii) Kupurukusha

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

iii) Mararu

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

## 2. MAKALA (Alama 15 )

### Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia

2. Mwelekeo wa utoaji mafunzo kwa walimu wa shule za sekondari nchini unazua mjadala. Hatua katika Nyanja hii zinaonekana kuchuliwa bila kutilia maanani utabiri wa idadi katika siku za usoni.

Hapo miaka ya tisini, walimu wengi waliohitimu katika shahada za digirii na diploma hawakuegemea upande wa Hisabati, Sayansi na Lugha (Kiingereza na Kiswahili). Hivyo kukazuka kampeni za chini kwa chini katika vyuo vya nchi ambapo walimu – wanafunzi walihimizwa kusomea Hisabati, Sayansi na Lugha. Hili lilionekana kuwa suluhu kwa wakati ule kwani punde baadaye walimu wote wa masomo haya walipewa marupurupu maalum maarufu kwa jina

“Special allowance” kwenye mishahara yao.

Idara za Dini, Historia na masomo mengine husika zilipuuzwa na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa hapa kupunguka kabisa. Wanafunzi katika idara hizi walionekana kutokuwa na matumaini ya kuajiriwa kwani wenzao waliokwisha kuhitimu walikuwa wengi kupindukia.

Hali hii ilidumishwa na miaka ya karibuni imeshuhudia tatizo linguine tofauti. Uhaba wa walimu wa Dini na Historia na ongezeko kubwa la walimu wa Hisabati, Sayansi na Lugha. Dalili zake ni ukweli kuwa wazi, hakuna wanaojitokeza kuzichukua. Miongoni mwa walimu waliohitimu na wanasaka nafasi za kazi, asilimia kubwa zaidi ni ya wa Hesabu, Sayansi na Lugha. Swali ni je kwa nini mambo yabadilike haraka jinsi hii?

Lawama zote zafaa kurundikiwa Wizara ya Elimu hasa idara zinazohusika na tarakimu na utoaji wa mafunzo kwa walimu. Kwa kufuatia njia za kitaalamu inawezekana kukadiria idadi ya walimu watakaohitajika katika masomo mbalimbali kwa kipindi cha miaka hamsini au hata zaidi. Maafisa katika idara hizi wafaa kuwajibika na kutoa mwelekeo thabiti ili kuiepushia nchi matatizo kama haya.

**Maswali**

a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno 50 – 60
MATAYARISHO
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

NAKALA SAFI

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 60 – 70.

MATAYARISHO

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

NAKALA SAFI

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )

3. a) i) Taja sauti ya king'ong'o cha kaakaa laini.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii) Andika sauti moja ya kipasuo kwamizo
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

b) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo. Umoja wa jamii hiyo umewawezesha kupigana na umaskini

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

c) Eleza miundo ya silabi katika neno lifuatalo.

Kichwa

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

d) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari

Yule mzembe alifika leo asubuhi

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

e) Ainisha shamirisho na chaagizo katika sentensi ifuatayo.

Wakulima walifanya kazi haraka sana kwa jembe.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

f) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kuleta dhana ya kujumuisha.

………………………………………………………………………………………………

g) Ainisha vielezi vya namna katitka sentensi ifuatayo. Wanafunzi wanaojikaza kisabuni hunyamaza jii darasani. …………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………………………

h) Tambua aina za nomino na utaje zimo katika ngeli zipi. Kuumia kwake kulisababishwa na kujikata kwa wembe. ……………………………………………………………………………………………

i) Chorea sentensi ifuatayo kielelezo cha matawi

Njoroge si mtiifu ingawa yeye ni mwerevu sana,

j) Eleza matumizi ya "kwa" katika sentensi ifuatayo.

Walivuka barabara kwa haraka wakienda kwao na sita kwa kumi wakagongwa kwa gari.
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

k) Eleza maana mbili zinazojitokeza kwenye sentensi ifuatayo.

Walimwibia Juma baiskeli.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

Mwalimu alitaka kujua kama wanafunzi wangeenda kumuona siku hiyo.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

m) Kanusha Wanafunzi watundu waliadhibiwa na kuaibishwa.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

n) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa

a. Oa……………………………………………… (tendesha)

b. Kokoa… ……………………………………… (tendata)

o) Tunga sentensi mojamoja kubainisha:

a. Kiwakilishi cha pekee chenye maana ya umilikaji.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

b. Kiwakilishi cha nafsi kiambata.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

p) Andika kinyume;

Shangazi angeingia tungemsifu.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

q) Tunga sentensi mojamoja kudhihirisha matumizi ya

a. “ka” ya mfululizo

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

b. “a” isiyodhihirika

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

r) Eleza matumizi mawili ya mabano.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

s) Onyesha kiima katika sentensi ifuatayo.

Wachezaji hao walicheza vizuri wakashinda.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

## 4. ISIMUJAMII (Alama 10 )

4. a) Eleza sababu tano za watu kuchanganya ndimi au kubadilimsimbo.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

b) Eleza umuhimu wa sajili za lugha.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………